# MABASHIRIO YA THAWABU DUNIANI NA AKHERA

<"xml encoding="UTF-8?>

BISMILAHI RAHMANI RAHIYMI
KWA JINA LA MWENYEEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.
MABASHIRIO YA THAWABU DUNIANI NA AKHERA.
6. Fungamano na uhusiano wa mabashirio ya thawabu duniani na Akhera.
Starehe na madhila ya Waumini duniani kwao wao ni sawa, kwa sababu hunufaika na starehe za duniani kwa neema za Mola wao, na hunufaika na mashaka ya duniani kwa kukumbuka mabashirio ya Mola wao, kwa sababu nyoyo zao hutulia pale wanapokumbuka mabashirio ya Mwenyeezi Mungu ambayo huwaondolea hofu, na nyoyo zao hufurahika wanapokumbuka ujira wa Mola wao. Kama tunavyosoma ndani -:ya Qur-ani

لَهُمُ الْبُشْرَي فِى الْحَياةِ الدُّنْيَا وَفِى الآخِرَةِ لاَ تَبْدِيلَ لِكَلِمَاتِ اللّهِ ذَٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ[1]
Wao wana bishara njema katika maisha ya dunia na katika Akhera. Hapana mabadiliko katika .maneno ya Mwenyezi Mungu. Huko ndiko kufuzu kukubwa

Vile vile wale watu ambao wanapigana jihadi kwa ajili ya Mwenyeezi Mungu, na wakawa* thabiti katika kukabiliana na Makafiri, basi Mwenyeezi Mungu Muweza atawanufaisha watu hao kwa kuwapa neema za ushindi na uhuru duniani, na siku ya Kiama atawaandalia ujira mkubwa wa pepo.
-:Katika Qur-ani tunasoma

فَآتَاهُمُ اللّهُ ثَوَابَ الدُّنْيَا وَحُسْنَ ثَوَابِ الآخِرَةِ وَاللّهُ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ[2]
Basi Mwenyezi Mungu akawapa malipo ya duniani na bora ya malipo ya Akhera. Na Mwenyezi Mungu anawapenda wafanyao mema.
Kwa hiyo, kutokana na maelezo hayo tumefahamu kuwa kuna uhusiano na fungamano baina ya utukufu, heshima, na uhakika wa bishara ya thawabu katika dunia na Akhera, na inapatikana kwa kumuamini Mola Muwezi. Kama tunavyosoma ndani ya Qur-ani .Majiyd

مَّن كَانَ يُرِيدُ ثَوَابَ الدُّنْيَا فَعِندَ اللّهِ ثَوَابُ الدُّنْيَا وَالآخِرَةِ وَكَانَ اللّهُ سَمِيعاً بَصِيرا[3]ً

Anaye taka malipo ya dunia, basi kwa Mwenyezi Mungu yapo malipo ya dunia na Akhera. Na*

Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia na Mwenye kuona.

7. Fungamano la viongozi, duniani na Akhera.

Viongozi wa jamii ni dalili bora na muhimu inayoonyesha uongofu na upotofu wa wanaadamu, kama inavyoeleweka kuwa mema na mazuri yote yanaonekana na kuthibitika kwa kuwafuata Maimamu wanaoitabua haki, na mabya na maovu yote yana uhusiano na Maimamu wanaofanya maovu na ukafiri. Kuna aina mbali mbali za watu katika dunia, aina hizo za watu ni kutokana na mapendeleo yao ya kiitikadi, na vigezo vya amali zao vitashuhudiwa kutoka kwa viongozi wao wa haki au wa kibatili, siku ya Kiama kutadhihirika fungamano la uwalii wa viongozi wema, na upotofu wa viongozi waovu, basi kila mmoja atavutwa ili amtafute .(kiongozi wake. Kama anavyosema Allah (s.w

يَوْمَ نَدْعُو كُلَّ أُنَاسٍ بِإِمَامِهِمْ فَمَنْ أُوتِيَ كِتَابَهُ بِيَمِينِهِ فَأُوْلَـئِكَ يَقْرَؤُونَ كِتَابَهُمْ وَلاَ يُظْلَمُونَ فَتِيلاً[4]

Siku tutapo waita kila kikundi cha watu kwa mujibu wa wakifuatacho - basi atakaye pewa kitabu chake kwa mkono wake wa kulia, basi hao watasoma kitabu chao wala hawatadhulumiwa hata chembe.

Siku ya Kiama viongozi waovu walio batili wataelekea motoni pamoja na wafuasi wao, kama -:tunavyosoma kuhusiana na Firauna

يَقْدُمُ قَوْمَهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فَأَوْرَدَهُمُ النَّارَ وَبِئْسَ الْوِرْدُ الْمَوْرُود[5]

Siku ya Kiyama atawatangulia watu wake na atawaingiza Motoni. Na muingio muovu ulioje huo!

Na Waumini pia wakiwa pamoja na Mitume na Maimamu wa haki wataelekea Peponi, na siku ya Kiama wataokoka na adhabu kali iumizayo, kama tunavyosoma -:ndani ya Qur-ani

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا تُوبُوا إِلَي اللهِ تَوْبَةً نَّصُوحاً عَسَي رَبُّكُمْ اَن يُكَفِّرَ عَنكُمْ سَيِّئَاتِكُمْ وَيُدْخِلَكُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِى مِن تَحْتِهَا الاَنْهَارُ يَوْمَ لاَ يُخْزِى اللهُ النَّبِيَّ وَالَّذِينَ آمَنُوا مَعَهُ نُورُهُمْ يَسْعَي بَيْنَ اَيْدِيهِمْ وَبِاَيْمَانِهِمْ يَقُولُونَ رَبَّنَا اَتْمِمْ لَنَا نُورَنَا وَاغْفِرْ لَنَا إِنَّكَ عَلـي كُلِّ شَيْءٍ قَدِير[6]

Enyi mlio amini! Tubuni kwa Mwenyezi Mungu toba iliyo ya kweli! Asaa Mola wenu Mlezi akakufutieni maovu yenu na akakuingizeni katika Pepo zipitazo mito kati yake, siku ambayo Mwenyezi Mungu hatamdhalilisha Nabii na walio amini pamoja naye. Nuru yao inakwenda mbele yao na pande zao za kulia, na huku wanasema: Mola wetu Mlezi! Tutimilizie nuru yetu, na utughufirie! Hakika Wewe ni Mwenye .uweza juu ya kila kitu

.Surat Yunus Aya ya 64 [1]

.Surat Al-Imrani Aya ya 148 [2]

.Suratun Nisaa Aya ya 134 [3]

Surat Israa Aya ya 71 [4]

Surat Hud Aya ya 98 [5]

.Surat Tahriym Aya ya 8 [6]

MWISHO